MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Mwandishi: C.E. Tatham

Everyday Publications Inc.
310 Killaly Street West
Port Colborne ON L3K 6A6
CANADA

Copyright © 1986 Everyday Publications Inc.

ISBN 0-88873-I25-6

Imprimé au Canada

Copyright © 1986 Everyday Publications Inc.

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Ukurasa

1. Imami 5
2. Ninaweza kujua namna gani ya kwamba nimeokolewa 9
3. Tabia zangu mbili 13
4. Uwezo wa Mungu ndani yangu 17
5. Ubatizo na karamu ya ukumbusho 20
6. Kukaa mbali na dunia 24
7. Maombi 28
8. Kanisa na Biblia 32
9. Makuhani wanaoabudu na kutumikia 36
10. Utumishi wetu kwa Bwana 40
11. Bwana atakuja tena 43
12. Taji na zawabu 47

Copyright © 1986 Everyday Publications Inc.

Copyright © 1986 Everyday Publications Inc.

- 1 -
IMANI
Tunaweza kuipata namna gani?

Ndani ya kitabu hiki tunataka kueleza nyingine za kweli kubwa ambazo inatupasa kujua na kufahamu kama tukitaka kupata nguvu katika imani. Petro alisema kweli hizi ni kama maziwa ya roho yasiyo na udanganyifu (1 Petro 2:2). Waamini wa kweli wameingia jamaa ya Mungu wakati walipozaliwa tena kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu na Neno la Mungu (Yoane 3:5; 1 Petro 1:23). Mungu Baba anataka wakae kujifunza kupita na kupita juu ya kweli yake. Wakati watu wanapozaliwa tena sasa tu wao ni kama watoto katika imani, lakini Mungu anataka wapate nguvu na kugeuka vijana, na nyuma ya wakati, hata baba (1 Yoane 2:12-14). Sharti usome polepole mashairi yote yanayotajwa ndani ya kitabu hiki, na kuomba Mungu kukusaidia kufahamu vizuri. Halafu mafundisho ya kitabu hiki yatakuwa na faida kubwa kwako.

Tuwaze kwanza juu ya neno kubwa moja, ndilo IMANI. Biblia inasema ya kwamba:

1. Zambi zetu zinasamehewa kwa njia ya imani ndani ya Kristo (Waroma 3:25).
2. Mungu anatuhesabia haki kama tukiwa na imani (Waroma 4:5).
3. Tumehesabiwa haki, maana yake, maneno yetu na Mungu yametengenea, kwa njia ya imani na sasa tuna salama naye (Waroma 5:1).
4. Tumeokolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani (Waefeso 2:8).
5. Hakuna mtu anayeweza kupendeza Mungu bila imani (Waebrania 11:6).

Mashairi haya na mashairi mengi mengine ndani ya Agano Jipya yanaonyesha ya kwamba imani ni neno kubwa sana. Shairi

Copyright © 1966 Everyday Publications Inc.

la mwisho tulilosoma, ndilo Waebrania 11:6, linaonyesha wazi ya kwamba ni lazima kwetu kuwa na imani kama tukitaka kupendeza Mungu. Hivi tunafahamu ya kwamba hatuwezi kujua Mungu bila imani.

Kwa sababu imani ni neno kubwa sana ni lazima kwetu kufahamu kama imani ni nini na kama tunaweza kuipata namnna gani.

Maneno YASIYO imani

Mara nyingine mtu anakubali na kinywa chake ya kwamba neno fulani ni kweli, lakini matendo yake hayapatani na masemo yake. Mtu huyu hana imani. Mfalme Agripa alikuwa hivi. Aliamini maneno Paulo aliyohubiri, lakini hakupokea Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wake (Matendo 26:27).

Watu wengine wanaamini maneno yote ambayo wanasikia, lakini kufanya hivi si imani ya kweli. Na wengine wanaamini maneno ya kushangaza hata kama inawashinda kuyafahamu.

Imani ni nini?

Kuwa na imani ni kuwa na hakika ya mambo yanayotumainiwa, kusadiki *mambo yasiyoonekana* (Waebrania 11:1).

Kwa kuweza kuwa na imani inapasa mtu:

1) kujua maneno Mungu anayokwisha kufunulia watu;
2) kuamini maneno haya na kukubali ya kwamba ni maneno ya kweli;
3) kupokea kwa yeye mwenyewe maneno haya yanayosema juu ya Bwana Yesu na kumwamini.

Inawezekana kwa mtu kujua na kuamini maneno Mungu anayokwisha kufunulia watu, lakini hapokei wokovu kama asipoamini Kristo, Kristo peke yake.

Kwa mfano tuwaze juu ya Petro. Siku moja Petro alitembea juu ya maji (Matayo 14:22-29). Bwana alisema naye kutembea juu ya maji na Petro aliamini ya kwamba Kristo aliweza kumchunga asizame ndani ya bahari. Alionyesha kwa njia ya matendo yake ya kwamba aliamini neno hili, akatoka chomboni na kuanza kutembea juu ya maji.

Imani

Mfano mwingine ni ndani ya Mwanzo 15:1-6:

1. Abrahamu alisikia masemo ya Mungu (sh. 4);
2. alijua kabisa ya kwamba Mungu aliweza kufanya neno ambalo aliahidi kufanya (sh. 5); na
3. aliamini Bwana (sh. 6).

Waza vilevile juu ya Paulo (Matendo 27:21-25).

1. Paulo alisikia habari toka Mungu kwa njia ya malaika (sh. 24).
2. Aliamini Mungu (sh. 25).
3. Alionyesha imani yake wakati alipowaambia watu wengine habari nzuri (sh.22).

Mtu anaweza kupata imani namna gani?

Wewe na mimi tunaamini maneno mengi na watu wengi. Kwa mfano, tunameza dawa fulani kwa sababu tunaamini dawa hii itatusaidia. Tunaingia motakaa kwa sababu tunaamini mwenye kuiongoza na ya kwamba atatufikisha pahali tunapotaka kwenda. Lakini hii si namna ya imani tunayohitaji kwa kuokolewa. Basi namna gani tunaweza kupata imani ya kuokoa roho?

Shairi 17 la sura 10 ya Waroma linatujulisha ya kwamba tunapata imani kwa njia ya kusikia Neno la Mungu. Lakini si lazima kwa sisi kulisikia na **masikio yetu** Tunaweza kusoma Neno la Mungu ndani ya Biblia au kitabu kingine. Isipokuwa hivi kiziwi hawezi kuokolewa!

Inatupasa kuamini nini?

Ndani ya Agano Jipya tunasoma juu ya Simoni Petro wakati alipokuwa na imani ndogo tu (Matayo 14:31); juu ya akida la Waroma aliyekuwa na imani **kubwa** (Matayo 8:10), na juu ya imani ya Abrahamu ambayo ilimpatisha **nguvu** (Waroma 4:20). Ni vizuri kabisa kwa mtu kuwa na imani ya nguvu kama Abrahamu, lakini neno kubwa zaidi ni kama tukiamini *nini* au *nani*. Kuwa na imani ndogo ndani ya dawa nzuri ni vizuri kupita kuwa na imani ya nguvu ndani ya dawa isiyo na faida. Sharti tutie imani yetu ndani ya Bwana Yesu Kristo na tutaokolewa (Matendo 20:21; Wakolosayi 1:4). Kama tukitumaini Kristo kabisa hatuko katika hatari ya kupotea tena. Noa na jamaa yake hawakuwa katika

hatari kwa sababu walikuwa ndani ya safina, si kwa sababu ya imani ya Noa tu. Noa aliingia safina kwa sababu aliamini na kutii Mungu.

Matunda ya imani ni nini?

Biblia inatupasha juu ya maneno mengi yaliyo matunda ya imani, lakini hapa tutataja maneno mawili tu:

1. **Mungu** anapendezwa wakati watoto wake walipo na imani (Waebrania 11:5-6). Anafurahi sana wakati tunapomwamini na kukubali Neno lake.
2. **Watu wanaokolewa na kuhesabiwa haki** wakati wanapoamini Kristo (Waroma 5:1; Waefeso 2:8-9; Matendo 26:18), na inapasa mwamini kuishi kwa imani (2 Wakorinto 5:7; Waebrania 10:38).

Soma mashairi haya na ujiulize kama mwenye imani alikuwa nani, mwanamume, mwanamke au mtoto:

Matayo 15:28 _____

Marko 5:34 _____

Luka 7:50 _____

- 2 -

Ninaweza kujua namna gani ya kwamba nimeokolewa?

Watu wengine wanasema ya kuwa wanajua wameokolewa. Hawana shaka hata kidogo ya kwamba Mungu amewaokoa na kuwapa uzima wa milele kwa sababu wanaamini Bwana Yesu.

Tunaweza kujua kabisa kabisa ya kwamba tuna uzima wa milele wakati tungali hapa duniani? Ndiyo, tunaweza. Mtume Yoane aliandika ya kwamba tunaweza kujua tumepita toka mauti kuingia uzima (1 Yoane 3:14). Paulo aliwaambia Wakristo wa Tesalonika ya kwamba aliwatangazia Habari Njema kwa sababu alijua kabisa ni habari za kweli (1 Watesalonika 1:5). Alijua ya kwamba watu wanaweza kuokolewa kama wakiamini Habari Njema.

Nani anaweza kujua hakika ya kwamba ameokolewa?

Watu wale tu walioamini Yesu. Watu hawa wamezaliwa tena kwa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu na wamegeuka watu wa jamaa ya Mungu (Yoane 1:12-13). Watu wengi wanategemea maneno mengine, si Kristo kuwaokoa, lakini wataona nyuma ya kwamba maneno haya hayawezi kuwaokoa. Kondoo za Bwana Yesu tu wanaweza kujua kabisa ya kwamba wana uzima wa milele na neno hili linawafurahisha kabisa (Yoane 10:27-28).

Namna gani mtu anaweza kujua kabisa ya kwamba ameokolewa?

Tuwaze kwanza juu ya maneno yasiyoweza kutusaidia kujua kabisa ya kwamba tuna uzima wa milele:

1. Furaha tunayosikia rohoni. Maneno mtu anayosikia rohoni au mwilini yanaweza kumdanganya. Mtu anaweza kujisikia vizuri mwilini pamoja na kuwa na ugonjwa mbaya. Mabikira watano wapumbavu ndani ya Matayo 25:1-13 walifikili wao ni

tayari kushiriki ndani ya karamu ya ndoa lakini waliachwa inje. Itakuwa vivyo hivyo na watu tunaosoma habari zao ndani ya Matayo 7:22-23 na Luka 13:25-27. Inawezekana kwa mtu kufikili ameokolewa wakati anapotegemea dini yake tu, si Kristo. Milioni za watu wamedanganywa kwa njia hii. Maneno mtu anayosikia rohoni mwake hayawezi kamwe kuhakikisha ya kwamba ana uzima wa milele, lakini mara nyingi mtu anayejua kabisa ya kwamba ameokolewa ana furaha vilevile.

Maneno haya yanafuatana hivi:

1. Tunajifunza ya kwamba sisi ni wenye zambi na Mungu ametutayarishia njia ya wokovu.
2. Tunaamini habari hizi na kupokea Krristo kuwa Mwokozi wetu.
3. Tunafurahi rohoni kwa sababu tunajua tumeokolewa.

2. *Kuwa mtu wa kanisa fulani au kutii maagizo ya dini yetu.* Maneno haya mawili hayawezi kutuokoa au kutusaidia kujua hakika ya kwamba tuna uzima wa milele. Saa wahubiri wengine wanapomaliza kuhubiri Habari Njema wanaomba watu wale wanaotaka kuamini kunyanyua mikono yao au kusimama, lakini neno hili haliwezi kufahamisha watu wale ya kwamba wameokolewa kweli. Labda kwa muda mfupi wata*sikia* rohoni mwao ya kwamba wameokolewa, lakini wakati wanapopata matata, wataanza kuwa na shaka kama waliokolewa kweli. Tusiache Shetani kutuaminisha ya kwamba tuna uzima wa milele wakati tusipoamini Kristo kweli.

Sasa tuone namna gani tunaweza kujua kabisa ya kwamba tumeokolewa kweli:

1. **USHUHUDA WA NENO LA MUNGU**. Mtume Yoane aliandika mashairi 9-12 ya 1 Yoane 5 ili tuweze kuamini jina la Mwana wa Mungu na kujua kabisa ya kwamba tuna uzima wa milele (1 Yoane 5:13). Sharti usome mashairi haya ndani ya Biblia yako. Tunaamini kila siku ushuhuda wa watu wakati tunapoamini maneno wanayosema. Basi inatupasa kuamini maneno Mungu anayosema yatatokea wakati tunapoamini Mwana wake. Mtu ye yote anayeamini Mwana wa Mungu ana uzima wa milele. Tunajua neno hili namna gani? Kwa sababu Mungu amesema hivi!

Ninaweza kujua namna gani ... ?

Abrahamu alijua kabisa ya kwamba Mungu atampa mwana hata kama yeye na mke wake walikuwa wazee. Basi Abrahamu alijua namna gani? Aliamini neno ambalo Mungu alimwambia (Waroma 4:20-21). Noa alijenga safina kujiponyesha mwenyewe pamoja na watu wa jamaa yake. Kwa nini alifikili kwamba kutakuwa na garika? Aliamini neno Mungu alilosema (Waebrania 11:7).

Rahaba alisihi wapelelezi kutoa kiapo ya kwamba Waisraeli hawataharibu jamaa ya baba yake, na aliwaomba kumpa kitu kuhakikisha ya kwamba watatimiza ahadi yao (Yosua 2:12). Walimpa nini? Ahadi yao. Waliahidi ya kwamba yeye na watu nyumbani mwake hawatakufa wakati baki la mji litakapoharibiwa. Rahaba aliamini maneno waliyosema, nao walitimiza ahadi yao (Yosua 6:22-23).

Malaika ya Bwana alipita katika inchi ya Misri kuharibu mwana mzaliwa wa kwanza ndani ya kila nyumba. Mungu alikataza malaika asiingie nyumba yo yote pahali baba alipokuwa ameweka damu juu ya mlango kwa upande wa inje. Wana wazaliwa wa kwanza walijua hawakuwa katika hatari ya kuuawa kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivi (Kutoka 12:13). Kwa sababu ya damu hawakuwa katika hatari; kwa sababu ya *Neno la Mungu* wali***jua*** ya kwamba hawakuwa katika hatari.

[Kufahamu kwa hakika kunaleta nini? Ona Wakolosayi 2:2.]

2. **USHUHUDA WA ROHO MTAKATIFU**. Tunasoma juu ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu kwa njia tatu ndani ya Agano Jipya:

Roho Mtakatifu auaTUshuhudia (Waebrania 10:15). Anatoa ushuhuda juu ya nini? Kazi Bwana Yesu Kristo aliyomaliza juu ya msalaba kwa ajili yetu, ndiyo kazi inayotosha kabisa kwa kutuokoa. Anatuambia ya kwamba waamini wanakamilishwa kwa milele kwa sababu ya zabihu ile (Waebrania 10:14).

> Roho Mtakatifu hatuambii mara nyingi juu ya kazi anayofanya ndani yetu; anatuongoza kufikili juu ya kazi ya Bwana Yesu Kristo kwa sisi.

Roho Mtakatifu anashuhudu PAMOJA NA roho zetu ya kwamba tuko watoto wa Mungu (Waroma 8:16). Mtu yule aliyezaliwa

tena anajua ya kwamba yeye ni mtoto wa Mungu na Roho Mtakatifu anasema hivi vilevile. Roho zetu na Roho Mtakatifu wanapatana ya kwamba tuko watoto wa Mungu.

> Tunafikili na kuhukumu maneno na roho zetu, lakini tunasikia furaha au huzuni na nafsi zetu. Tujikumbushe tena ya kwamba ushuhuda wa Roho Mtakatifu unafungana na ule wa roho zetu, si ule wa mwili au nafsi yetu.

Ushuhuda wake NDANI yetu. Watu wale wanaoamini Mwana wa Mungu wana ushuhuda wa Roho Mtakatifu ndani yao kuwajulisha ya kwamba faida ya mauti ya Kristo inatosha kwa milele (1 Yoane 5:10).

Wale wanaoamini Mwana wa Mungu wana ushuhuda wa inje vilevile, ndio Neno la Mungu. Wana ushuhuda *ndani* yao, ndio ushuhuda wa Roho Mtakatifu. Ushuhuda huu wa Roho Mtakatifu si mbali kabisa na Neno la Mungu kwa sababu Roho Mtakatifu atatumia Neno la Mungu kusema na mioyo na zamiri zao.

- 3 -
Tabia zangu mbili

Kama tukitaka kuendelea na kupata nguvu katika imani yetu inatupasa kufahamu ya kwamba tuna tabia mbili. Wakati tunapozaliwa hapa duniani tunapokea tabia ya zamani, ya zambi, inayoitwa mwili vilevile. Tunapokea tabia mpya wakati tunapozaliwa tena. Tabia hii mpya inaitwa *roho* vilevile. Bwana Yesu alieleza neno hili wazi wakati aliposema, "kilichozaliwa kwa Roho ni roho" (Yoane 3:6).

Ndani ya Biblia neno hili "mwili" lina maana mbili. Mara nyingine linasema juu ya mwili wenye viungo, ndiyo mikono na miguu, kama ndani ya Yoane 3:6. Mara nyingine maana yake ni tabia yetu ya zambi tuliyopokea sisi sote kwa sababu tuko wazao wa Adamu. Ndani ya somo hili tutawaza juu ya maana hii ya pili.

Neno hili *roho* linatumiwa kwa roho ya mtu. Kila mtu ana mwili, nafsi na roho (1 Watesalonika 5:23). Tabia mpya inaitwa roho vilevile kwa sababu ni mbalimbali na mwili.

Utafahamu tofauti katikati ya tabia hizi mbili wakati utakaposoma mashairi haya:

Mwili	**Roho**
Yoane 3:6	Yoane 3:6
Waefeso 4:22	Waefeso 4:24
Waroma 7:23	Waroma 7:22
Waroma 8:7-8	2 Petro 1:4

Tabia hizi mbili zinashindana saa zote. Tabia yetu ya zamani inashindana na maneno tabia mpya inayotaka, na tabia mpya haitaki maneno tabia ya zamani inayotamani. Tabia hizi mbili zina uadui, na kwa sababu hii hatuwezi kufanya maneno tunayotaka kufanya (Wagalatia 5:17).

Waamini wengi wa sasa wanashindwa na zambi kwa sababu hawafahamu vizuri:

1) kama mwili ni nini
2) kama uzima mpya ni nini

3) namna gani wanaweza kuishi maisha ya kushinda.

Tuangalie mafundisho ya Maandiko Matakatifu juu ya maneno haya:

1. Mwili

Hakuna neno linaloweza kutengeneza mwili, ndio tabia ya zambi. Ndani ya Yerernia 17:9 tunasoma ya kwamba rnioyo yetu ni miovu sana na haifai kwetu kuitegemea. Mawazo maovu yanatoka kwa moyo wa mtu, na mawazo haya yanamwongoza kufanya maneno maovu mengi (Marko 7:21-23). Mwili ni adui wa Mungu na hatii sheria zake—hawezi kuzitii. Watu wengine wanafanya mapenzi ya tabia yao ya zamani; na hawawezi kupendeza Mungu (Waroma 8:7-8). Ndani ya Yoane 6:63 tunasoma ya kwamba mwili hauna faida hata kidogo. Mtu asiyeokolewa bado hawezi kutii, kupendeza au kufahamu Mungu (Waefeso 2:3; 1 Wakorinto 2:14).

Tabia yetu ya zambi haituondokei wakati tunapozaliwa tena. Haya ndiyo mafundisho ya Biblia na tunaona ya kwamba ni kweli. Paulo alijua ya kwamba tabia yake ya zamani ikuwa mbaya kabisa (Waroma 7:18), naye alitukataza tusifanye neno lo lote kushibisha mahitaji ya mwili (Waroma 13:14). Asingalisema hivi kama tusingalikuwa na tabia ya zambi nyuma ya kuokolewa.

Tabia ya zamani haigeuki kuwa nzuri kupita wakati tunapookolewa. Mwili unaweza kuzaa matendo ya mwili tu (Yoane 3:6). Tabia ya zamani haiwezi kamwe kugeuka tabia mpya. Ina uadui na Mungu (Waroma 8:7), na ni kama nyuma ya kuokolewa kwa mtu, tabia yake ya zamani ni hata mbaya kupita mbele. Ni kwa sababu Roho Mtakatifu amekuja kukaa ndani ya mtu huyu na anafunua uovu wa mwili. Uovu wake haupunguki hata ndani ya Mkristo wa miaka mingi. Labda mwili unajionyesha kwa njia nyingine ndani ya Mkristo, lakini ni mwili tu kama mbele.

Wana wawili wa Abrahamu ni mfano wa tabia mbili. Isimaeli ni mfano wa mtu wa mwili, wa dunia, mwenye tabia ya zambi. Isaka ni mfano wa mtu wa roho, mwenye tabia mpya. Isimaeli hakuleta matata nyumbani mara moja, lakini wakati Isaka alipozaliwa, vita ilianza (Mwanzo 21:9). Vivyo hivyo tabia yangu ya zamani hainisumbushi kufika wakati

ninapopata tabia mpya.

2. Tabia mpya

Mtoto wa kweli wa Mungu hakai kufanya zambi kwa sababu ana tabia ya Mungu ndani yake. Hawezi kuendelea ndani ya zambi kwa sababu Mungu ni Baba yake (1 Yoane 3:9). Ona maneno matatu juu ya tabia mpya:

1) *Tabia mpya inatoka kwa Mungu.* Tulipokea tabia ya zamani toka Adamu wakati tulipozaliwa hapa duniani na tunapokea tabia mpya toka Mungu wakati tunapozaliwa tena. Tabia ya zamani ni mbaya kabisa lakini tabia mpya ni nzuri kabisa. Inaitwa vilevile tabia ya Mungu (2 Petro 1:4).

2) *Tabia mpya haiwezi kufanya zambi* (1 Yoane 3:9; 5:18). Neno hili ni kweli kwa waamini wote wa kweli, si kwa waamini wachache tu wanaotembea karibu zaidi na Mungu. Si kusema ya kwamba mwamini hafanyi zambi kamwe (ona 1 Yoane 2:1), lakini ya kwamba hadumu ndani ya zambi. Tabia ya Mungu mwenyewe ni ndani ya Mkristo, na tabia hii haiwezi kufanya zambi. Mti unaweza kuzaa matunda ya namna yake tu, kwa mfano mtini unaweza kuzaa tini tu, hakuna matunda mengine (Yakobo 3:12). Vivyo hivyo tabia ya Mungu ndani yangu inaweza kuzaa matunda mazuri tu.

Soma Waroma 8:8 na 1 Yoane 3:9 na sawanisha mashairi haya mawili:

Neno gani haliwezekani ndani ya 1 Yoane 3:9? _____

Neno gani haliwezekani ndani ya Waroma 8:8? _____

3) *Tabia mpya inafurahia maneno ya Mungu.* Paulo alisema alifurahia sheria ya Mungu kwa mtu wa ndani (Waroma 7:22). Tabia mpya inasukuma mwamini kuomba Mungu, kama Paulo alivyofanya (Matendo 9:11); na kujilisha na Neno la Mungu kama mtoto mchanga (1 Petro 2:2). Wenye tabia mpya wanapenda waamini wengine (1 Yoane 3:14), na neno hili linatusaidia kujua ya kwamba wameokolewa.

Namna gani Mkristo anaweza kuishi maisha ya kushinda?

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Kuna Wakristo namna mbili: wale wanaofanya maneno tabia ya zamani inayotaka wafanye, na wale wanaotii tabia mpya. Soma 1 Wakorinto 3:1-4 na 2:15.

Namna gani tunaweza kutii tabia mpya na kugeuka Wakristo wanaofuata Bwana karibu karibu? Tutajibu ulizo hili sasa na ndani ya Somo 4 vilevile.

Mungu alihukumu zambi zangu wakati Bwana Yesu Kristo alipokufa juu ya msalaba. Zambi hizi ni matunda ya tabia yangu ya zamani, ya zambi. Anasamehe zambi zangu lakini anahukumu tabia yangu ya zambi. Inanipasa kufanya vivyo hivyo kama nikitaka kumpendeza. Waza juu ya mashairi haya matatu:

1) Wafilipi 3:3 linatupasha ya kwamba haifai tutegemee mwili au maneno yo yote sisi tunayoweza kufanya. Mwili ni mbaya na hautazaa kamwe neno litakalopendeza Mungu.

2) Waroma 13:14 linatukataza tusifanye neno lo lote litakalotimiza tamaa ya tabia yetu ya zambi.

3) Ndani ya Waroma 8:13 tunaagizwa kuua matendo ya mwili, rnaana yake kujihukumu wenyewe. Tukijihukumu wenyewe, na zambi zetu, tutaishi maisha ya kushinda (1 Wakorinto 11:31).

Ilipasa Waisraeli kukata miili yao na visu vikali mbele ya kuweza kutumaini ya kwamba wataweza kushinda watu wa inchi ya Kanana. Walitumia visu hivi vikali kwa Gilgali, ndipo pahali palipogeuka kambi ya majeshi wenye kushinda wa Israeli (Yosua 5:2-3,9; 10:23). Neno hili ni mfano wa Mkristo ambaye anajihukumu mwenyewe na zambi zake na anayeishi maisha ya kushinda nyuma yake.

Tunaweza kufanya maneno haya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tu. Tutasoma zaidi juu yake ndani ya Somo 4.

- 4 -

Uwezo wa Mungu ndani yangu

Tumesoma mashairi matatu yanayoonyesha namna gani tunaweza kushinda tabia yetu ya zamani, tabia ya zambi. Mashairi haya ndiyo Wafilipi 3:3, Waroma 13:14 na 8:13. Sorna mashairi haya tena na ona kama mawili yao yakisema nini juu ya Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu tu anaweza kutupa sisi uwezo kuishi narnna inavyopasa Mkristo kuishi. Kujua tu ya kwamba Mungu amesamehe zambi zangu hakutanisaidia kushinda majaribu au zambi. Nikitaka kushinda, inanipasa kupata kusaidia toka Kristo anayetukuzwa sasa mbinguni. Msalabani Mwokozi alipata azabu kwa zambi zangu. Sasa amefufuliwa toka wafu, na wakati ninapokaa kumtazama yeye, Roho Mtakatifu ananifungua toka uwezo wa zambi. Kristo alifanya kazi yake kwa mimi. Sasa Roho Mtakatifu anafanya kazi yake ndani yangu. Biblia inafundisha nini juu ya Roho Mtakatifu wa Mungu?

Roho Mtakatifu ni kama mtu kwa njia nyingine. Anaishi ndani ya mwamini na uwezo wake unaweza kusaidia Mkristo kuishi kwa Mungu. Tuwaze juu ya maneno haya:

Roho Mtakatifu ni kama mtu.

Roho Mtakatifu ni Mungu. Yeye ni wa milele na ni kipimo kimoja na Mungu Baba na Mungu Mwana (Matayo 28:19; 2 Wakorinto 13:14; Waebrania 9:14). Maneno yote yaliyo kweli juu ya Mungu ni kweli juu ya Roho Mtakatifu vilevile. Mashairi yanayofuata yanafundisha nini juu ya Roho Mtakatifu? Andika jibu lako juu ya mstari kwa kuume wa shairi lenyewe.

Matayo 12:28 _____

1 Wakorinto 2:10 _____

Zaburi 139:7-10 _____

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Waebrania 10:29 _____

Roho Mtakatifu ana*fundisha* (Yoane 14:26); ana*sema* (Wagalatia 4:6); ana*ongoza* (Wagalatia 5:18; Waroma 8:14); anatu*ombea* mbele ya Mungu (Waroma 8:26); na anaweza *kuwa na huzuni* (Waefeso 4:30). Haya ndiyo machache ya mashairi yanayohakikisha ya kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu.

Roho Mtakatifu anaishi ndani ya mwamini

Mbele ya siku ya Pentekote Roho Mtakatifu alikuja juu ya watu fulani, lakini hakukaa ndani yao (Yoane 7:39). Halafu siku ya Pentekote kuja kwa Roho Mtakatifu kulikuwa namna nyingine (Matendo 2). Kwa wakati wa sasa anaishi ndani ya kila mwamini wa kweli, si kwa sababu Mkristo huyu amefanya kazi fulani kwa Mungu, lakini kwa sababu ameamini Bwana Yesu Kristo. Mungu alituma Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu kuonyesha ya kwamba tuko wana wake (Wagalatia 4:6). Soma mashairi haya vilevile: 1 Wakorinto 6:19; 12:13; 2 Wakorinto 1:21-22. Agano Jipya linafundisha waziwazi ya kwamba Roho Mtakatifu anaishi ndani ya kila mwamini wa kweli (Waroma 8:9). Mungu Baba ametupa sisi Roho Mtakatifu kuhakikisha ya kwamba sisi ni mali yake (Waefeso 1:13; 1 Yoane 2:18,20).

Roho Mtakatifu anaishi ndani ya waamini wote wa kweli, lakini si waamini wote wanaojazwa Roho Mtakatifu. Mungu anatuagiza kujazwa na Roho Mtakatifu (Waefeso 5:18). Tunaweza kutii agizo hili namna gani?

Tukitaka kujazwa na Roho Mtakatifu inatupasa kujihukumu mbele ya Mungu, kujitoa kwake kwa kufanya mapenzi yake, na kumpa Bwana Yesu pahali pa kwanza ndani ya maisha yetu.

Uwezo wa Roho Mtakatifu

Tunahitaji uwezo wa Roho Mtakatifu kwa kutufungua toka sheria ya zambi na kufa (Waroma 8:2), na kwa kutuwezesha kushuhudia Kristo. Tunaweza kuwa na uwezo huu kama tukilisha roho zetu na Neno la Mungu na kuongozwa na Roho Mtakatifu ndani ya maombi yetu (Yuda 20; Waefeso 6:18).

Unataka Roho Mtakatifu kukufungua toka sheria ya zambi?

(Waroma 8:2). Unataka Roho Mtakatifu kukusaidia kushuhudia Bwana bila woga? (2 Timoteo 1:7). Atafanya hivi kama ukijitoa kwa Mungu na kufanya mapenzi yake aliyofunua ndani ya Neno lake.

Roho Mtakatifu anatusaidia kutukuza Mungu.

Haifai tufanye maneno ambayo tabia yetu ya zamani inatusukuma kufanya. Sharti tuache Roho Mtakatifu kutuongoza na kutawala maisha yetu (Wagalatia 5:16, 25). Tukifanya hivi tutajuana na Mungu vizuri kupita na kupita na kumtukuza kila siku. Watu wengine wataweza kuona Bwana Yesu ndani yetu, si neno kama tukiwa pahali gani, au darasani, au nyumbani, au kwa pahali pa kazi.

Roho Mtakatifu anatusaidia kushuhudia Kristo.

Tunahitaji uwezo wa Roho Mtakatifu kwa kujulisha watu wengine habari za Kristo. Bwana Yesu aliahidi wanafunzi wake ya kwamba watapokea Roho Mtakatifu, kisha watamshuhudia pahali pote duniani (Matendo 1:8).

Soma mashairi haya na andika majina ya watu waliojazwa Roho Mtakatifu:

Luka 1:67 _____

Matendo 1:8 _____

Matendo 2:4 _____

Matendo 4:8 _____

Matendo 4:31 _____

Vizuri sisi vilevile tujazwe Roho Mtakatifu ili watu waweze kuona Kristo ndani yetu na kutukuza Mungu.

- 5 -

Ubatizo na Karamu ya Ukumbusho

Mungu aliwapa Wayuda sheria nyingi za dini lakini aliagiza Wakristo maneno mawili: UBATIZO, na KARAMU YA UKUMBUSHO. Maneno haya mawili ni kwa waamini tu na yanatukumbusha mauti ya Kristo msalabani. Mungu alikusudi maneno haya kufunganisha Wakristo pamoja, zaidi karamu ya ukumbusho (1 Wakorinto 10:17), lakini Shetani ameyatumia kututenga.

Ubatizo na Karamu ya Ukumbusho ni mambo makubwa kwa sababu ni mifano ya mauti ya Bwana Yesu kwa ajih yetu.

UBATIZO

Tuone kama maana ya ubatizo ni nini, namna gani inapasa watu kubatizwa, na kama inapasa watu gani kubatizwa.

Maana ya ubatizo

Maandiko Matakatifu yanafundisha ya kwamba tulikufa parnoja na Kristo wakati alipokufa juu ya msalaba (Warorna 6:6).

Kuna njia moja tu kwa mtu kutoka ndani ya jamaa yo yote, ndiyo kufa; tulitoka jamaa ya Adamu wakati tulipokufa pamoja na Kristo. Sasa tuko watu wa jamaa ya Mungu.

Lakini tulikufa *namna gani*? Ndani ya Mkombozi wetu mkamilifu, ndiye Bwana Yesu Kristo. Ubatizo ni mfano wa kweli hii, mfano wa mtu anayekufa, na kuzikwa. Ona Waroma 6:1-4 na Wakolosayi 2:12.

Maneno haya yanaonyesha wazi kabisa ya kwamba inapasa waamini wa kweli tu kupata ubatizo kwani wao tu wamekufa pamoja na Kristo.

Ubatizo

Inapasa watu kubatizwa namna gani?

Maandiko Matakatifu yanafundisha ya kwamba sharti mwili mzima wa mtu uwekwe chini ya maji saa anapobatizwa. Kwa sababu gani?

1. *Maana ya neno hili "batiza" ndani ya lugha ya Agano Jipya.* Ndani ya lugha ile maana ya neno hili ni kuingiza kitu kizima ndani ya maji, au kuteka maji kwa njia ya kuweka chungu ndani ya maji kwa kukijaza.

2. *Ubatizo ni mfano wa mtu akizikwa*. Hatuweki udongo nusu tu juu ya maiti lakini tunaingiza maiti nzima ndani ya kaburi na kuifunika kabisa na udongo kufika saa isipoonekana tena.

3. *Mifano ndani ya Agano Jipya.* Filipo alifundisha towashi namna gani aliweza kuokolewa na towashi alitaka kubatizwa mara moja. Wanaume wale wawili waliingia ndani ya maji na Filipo alimbatiza (Matendo 8:38-39). Wasingalihitaji kufanya hivi kama Filipo angaliweza kubatiza towashi kwa njia ya kumnyunyizia nusu ya maji tu kichwani.

Yoane Mbatizaji alibatiza watu katika Ainoni kwa sababu maji yalikuwa mengi kule (Yoane 3:23). Asingalihitaji maji mengi kama angaliweka maji nusu tu juu ya kichwa cha kila mtu!

Inapasa watu gani kupata ubatizo?

Ndani ya Agano Jipya waamini tu walibatizwa. Walikuwa
wanafunzi, Matayo 28:19;
waamini, Marko 16:16;
watu wa kukomea, Matendo 8:12;
watu waliokwisha kupokea Roho Mtakatifu, Matendo 10:47.

Soma vilevile sura hizi ambazo zinatupasha juu ya watu wengine waliobatizwa. Andika hesabu ya shairi ndani ya kila sura linalosema ya kwamba walikuwa waamini:

Matendo 16:_____

Matendo 18:_____

Matendo 19:_____

KARAMU YA UKUMBUSHO

Soma mashairi haya polepole: Matayo 26:26-30; Marko 14:22-26; Luka 22:19-20; Matendo 20:7; 1 Wakorinto 10:16-17; 11:23-30. Haya ndiyo mashairi yote ambayo yanatupasha juu ya karamu ya ukumbusho. Tutafute majibu kwa maulizo matatu juu ya karamu hii:

Inatupasa kuvunja mkate KWA SABABU GANI?

Kwa sababu Bwana Yesu alituomba kufanya hivi. Ni neno la mwisho aliloomba usiku ule Yuda alipomtoa kwa adui zake. Hatufikili juu yake kama neno ambalo alitu**agiza** kufanya, lakini kama neno ambalo alitu**omba**. Bwana Yesu alisema ya kwamba wale ambao wanampenda hawatatii maagizo yake tu lakini **masemo** yake vilevile; maana yake watafanya neno lo lote alilosema litamfurahisha (Yoane 14:23). Wakati alipokwisha kurudi mbinguni aliomba waamini kwa njia ya Paulo kumkumbuka yeye kwa njia hii (1 Wakorinto 11:23-24). Hivi tunavunja mkate kwa sababu Bwana wetu alituomba kufanya hivi na kwa sababu tunataka kumpendeza.

Inapasa NANI kuvunja mkate?

Watu wale tu wanaojua Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wao. Tunavunja mkate kukumbuka Bwana wetu lakini hatuwezi kukumbuka mtu ambaye hatumjui. Bwana Yesu alisimamisha karamu hii kwa waamini tu na ndani ya Agano Jipya waamini tu waliishika. Haifai hata kidogo kwa mtu kula mkate na kunywa toka kikombe bila kufahamu maana ya neno ambalo anafanya (1 Wakorinto 11:29).

Wakristo wengine wanadumu ndani ya zambi na wengine wanafundisha maneno mabaya. Haifai Wakristo hawa kula karamu ya ukumbusho. Ona 1 Wakorinto 5:11-13 na 2 Yoane 10-11.

Inatupasa kuvunja mkate NAMNA GANI?

Inatupasa kuvunja mkate pamoja na Wakristo wengine, si peke yetu. Ndugu za kanisa wanakutana pamoja wakati na wakati (1 Wakorinto 11:26) kwa jina la Bwana Yesu tu (Matayo 18:20) kula

karamu ya ukumbusho. Mtu ye yote anaweza kukumbuka Bwana kwa njia ya kula karamu hii kama alizaliwa tena na kuwa ndani ya mwili wa Kristo (1 Wakorinto 12:12). Mkate mmoja juu ya meza ni mfano wa mwili huu (1 Wakorinto 10:17), na waamini wote ni viungo vya mwili wa Kristo. Mkate ni mfano vilevile wa mwili ambao Bwana Yesu alikuwa nao hapa duniani, na kikombe ni mfano wa damu yake ya damani ambayo alimwanga.

Hivi tunakula mkate nusu na kunywa nusu toka kikombe kwa kukumbuka zabihu Bwana Yesu aliyotoa juu ya msalaba wakati alipojitoa mwenyewe kwa zambi zetu. Roho zetu zinajaa na kuabudu wakati tunapowaza juu ya Bwana wetu na taabu yote aliyopata kwa ajili yetu. Kusudi la kusanyiko hili si maombi au kujifunza Neno la Mungu, lakini kuabudu Bwana wetu. Hakuna mtu fulani aliye kiongozi cha kusanyiko hili lakini ingepasa mwanamume ye yote kuweza kuongoza ndugu wengine ndani ya kuabudu, akiongozwa yeye mwenyewe na Roho Mtakatifu.

- 6 -

Kukaa mbali na dunia

Bwana anaagiza kila mwamini kujitenga na maneno yote yasiyo safi. Tunaona neno hili ndani ya 2 Wakorinto 6:17 na ndani ya mashairi mengi mengine. Wakristo wanaotii agizo hili ndio Wakristo wa pekee wenye furaha ya kweli. Shetani hataki kamwe kwa Wakristo kujiweka mbali kwa Mungu. Anajaribu wakati wote kugawa maneno Mungu anayotaka kufunga pamoja na kufunga pamoja maneno Mungu anayotaka kuwa mbalimbali. Kwa mfano, Mungu anataka waamini wote wa kweli kuwa rnoja, lakini Shetani anajua ya kwamba Wakristo wana nguvu nyingi kama wakiwa moja. Amegawa waamini kwa njia ya kuwapa mawazo mbalimbali juu ya mafundisho ya Biblia. Na Mungu anataka Wakristo kujitenga na wasioamini, lakini Shetani anajaribu sana kuzuiza neno hili vilevile.

Ndani ya Waroma 12:2 tunasoma ya kwamba haifai kwetu kufananishwa kwa namna ya dunia hii. Roho Mtakatifu anataka tufahamu kama maana ya "dunia" ndani ya shairi hili ni nini. Soma 1 Yoane 2:16 na andika maneno matatu yaliyo ya dunia.

1) _____

2) _____

3) _____

Ndani ya 1 Yoane 5:19 tunaona ya kwamba dunia nzima inatawaliwa na Shetani. "Dunia" ndiyo watu na pahali na maneno yote yanayofanywa bila kukumbuka Mungu.

Roho ya watu wa dunia ilionekana wazi kwa msalaba wa Kristo wakati walipolalamika, "Ondosha mtu huyu. . . umsulibishe, umsulibishe" (Luka 23:18, 21). Watu wa dunia hii walisulibisha Mwokozi wetu na hawakutubu zambi hii kamwe. Kwa

sababu hii Mungu amehukumu dunia hii nayo itaharibiwa wakati Kristo atakaporudi kama Mwamuzi (Matendo 17:31; Ufunuo 19).

Mungu Baba ameondosha Mkristo duniani. Ndiyo, milii yetu ingali hapa lakini hatuko wa dunia tena (Yoane 15:19; 17:6). Bwana Yesu Kristo anatutuma katika dunia tuweze kumshuhudia (Yoane 17:18), hata kama sisi si watu wa dunia (Yoane 17:16). Inatupasa kukaa kama wageni na wasafiri hapa duniani (1 Petro 2:11).

Mifano ya kujitenga ndani ya Agano la Kale

Kuna mfano wa mtengano ndani ya sura ya kwanza ya Biblia: Mungu alitenga nuru na giza (Mwanzo 1:4). Soma vilevile Walawi 19:19 na Torati 22:9-11.

Mungu alikataza Waisraeli wasifanye maneno matatu:

1) Hawakuwa na ruhusa kupanda mbegu namna mbali-mbali ndani ya shamba moja.
2) Hawakuwa na ruhusa kufunga ngombe ndume na punda pamoja kukokota jembe. Ngombe alikuwa nyama safi na punda alihesabiwa kuwa nyama mchafu (Walawi 11:4-8).
3) Hawakuwa na ruhusa kuvaa vazi lililofanywa la nguo namna mbili kama sufu na kitani.

Mashairi haya yanatufundisha ya kwamba Mungu hataki tuchanganye maneno yaliyo mbalimbali.

Mungu yeye mwenyewe alitenga Waisraeli na Wamisri (Kutoka 11:7), na alikataza Waisraeli wasioane na watu wa mataifa ambao waliwazunguka (Torati 7:3-4).

Mungu anaagiza Wakristo kujitenga na dunia

Haiwezekani kwa mtu kutumikia bwana wawili pamoja. Hatuwezi kutumikia Mungu na mali pamoja (Matayo 6:24). Paulo alitukataza tusiwe na maneno hata kidogo na watu wanaofanya zambi au maneno yasiyo na faida, lakini kuyahamakia (Waefeso 5:11). Aliagiza Wakristo vilevile kuacha uovu (2 Timoteo 2:19). [Namna gani tunaweza kupenda dunia na Mungu Baba vilevile? Ona 1 Yoane 2:15.]

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Kuna mashairi mengi mengine yanayofundisha kweli hii lakini mashairi haya tunayokwisha kutaja yanatosha kuonyesha ya kwamba Mungu anataka waamini kukaa mbali na dunia hii inayokataa Bwana wao. Haifai kwa Wakristo kufungana pamoja na wasioamini. kwa maneno ya anasa, ndoa, kazi, au kuabudu Mungu. Si kusema ya kwamba inapasa Wakristo kuhama na kukaa pahali pengine peke yao. Sharti tupange katikati ya watu wa dunia hii ili tuweze kuwapasha Habari Njema, lakini haifai tufanye mapatano nao.

Maneno ya dunia ni namna mbali: 1) maneno yale yaliyo zambi, na 2) maneno yasiyo na faida. Ndiyo, zambi ni mbaya kila mara na maneno yasiyo na faida yanageuka zambi vilevile kama tukiweka saa na roho zaidi juu yao.

Wakristo wanauliza mara nyingi kama neno fulani ni zuri au sivyo. Biblia haionyeshi waziwazi kama ni vizuri kwa sisi kulifanya au sivyo. Basi tufanye nini juu ya maneno ya namna hii? Kuna maneno mane tunayoweza kuuliza kwa kupima maneno haya:

1. Neno hili ni kwa utukufu wa Mungu? Ona 1 Wakorinto 10:31.
2. Nikifanya neno hili, nitaasi agizo lo lote la Maandiko Matakatifu?
3. Neno hili litakuwa na faida kama nikililfanya?
4. Ninaweza kuomba Mungu kulibariki?

Majibu yetu kwa maulizo haya yatatufahamisha wazi kama ni neno zuri au baya.

Matunda ya kujitenga na dunia

Wakristo ambao wanajitenga na dunia wanabarikiwa na upatano wa karibu na Bwana na uwezo toka kwake. Labda inaonekana kwa watu wengine ya kwamba hawaendelei vizuri sana hapa duniani, lakini Mungu ameahidi maneno matatu ya ajabu kabisa kwa sababu wanatii agizo la 2 Wakorinto 6:14-16. Soma mashairi haya.

1. *Anaahidi kuwapokea*. Aliwapokea mbele kama wenye zambi (Luka 15:2), lakini sasa anawapokea kama watakatifu kufurahi ndani ya upatano mtamu naye.

Kukaa mbali na dunia

2. *Anaahidi kuwa Baba kwao*. Mwamini ambaye anajitenga na dunia anajua ya kwamba Mungu ni Baba yake na neno hili lina-mfurahisha sana.

3. *Yeye Bwana Mwenyezi anasema ya kwamba watakuwa wana na binti kwake.* Maana ya jina hili kwa Mungu, **Mungu Mwenyezi**, ni ya kwamba kwa uwezo wake Mungu atalinda watoto wake wenye kumtii na atawasaidia kumtumikia. Ndani ya Agano la Kale tuna-soma juu ya waamini wengine wasiotii agizo hili kujitenga na dunia.

Loti alikuwa mtoto wa Mungu (ona 2 Petro 2:7-8), lakini alikuwa na ushirika na urafiki na watu waovu wa Sodomo (Mwanzo 19).

Solomono alifungana na wanawake wapagano na kuoa wengi wao lakini walimkokota mbali na Mungu (1 Wafalme 11:1-4).

Yosafati alifanya mapatano ya biashara na mfalme mwovu, ndiye Ahazia. Mwisho wake ulikuwa nini? Alipoteza merikebu zake zote na baraka za roho vilevile (2 Mambo 20:35-37).

Inawezekana kwa sisi kuwa na upatano wa karibu na Bwana Yesu Kristo. Kama tukiwa na upatano wa namna hii, tutakataa maneno yote watu wa dunia wanayotaka kutupa sisi kwa sababu Bwana Yesu Kristo mwenyewe anatupa vyote tunavyohitaji kwa miili na roho zetu.

- 7 -

Maombi

Zaidi ya watu wa dunia wanaombaga hata kama wengi wao hawajui NAMNA GANI inawapasa kuomba. Neno hili linaonyesha ya kwamba watu wana roho nao ni namna nyingine na nyama. Mara nyingi mtu analilia Mungu kumsaidia wakati anapopata taabu lakini nyama hawafanyi hivi. Hata wasioamini wanaomba Mungu wakati wa matata, na mara nyingine Mungu anajibu rnaombi yao na kuwaponyesha. Alifanya hivi na wabaharia waliotupa Yona ndani ya bahari (Yona 1:14-16). Mungu anasikia maombi ya watu wote wakati wanapoomba na kukiri zambi zao mbele yake (Zaburi 65:1-2). Lakini waamini wa kweli tu wanaweza kuomba kwelikweli kwa Baba yao, Mungu mwenye mapendo na uwezo wote.

Mifano ya maombi

Kuna mifano mingi ya maombi ndani ya Agano la Kale na Agano Jipya. Watu walianza kuomba Mungu kwa wakati wa Seti (Mwanzo 4:26), na ndani ya sura ya mwisho ya Biblia tunasoma ya kwamba Roho Mtakatifu na Bibi Arusi (Kanisa) wataomba Mwokozi kurudi (Ufunuo 22:17, 20). Kwa wakati wa Agano la Kale manabii waliomba, na makuhani na wafalme walifanya vivyo hivyo.

Nani alikuwa akiomba ndani ya mashairi haya? Andika majina yao juu ya mistari kwa kuume.

1 Samweli 12:23 _____

Hesabu 6:24-26 _____

1 Mambo 17:25 _____

Abraharnu aliomba, na viongozi wote wa taifa la Israeli walifanya vivyo hivyo, ndio Musa, Yosua, Solomono, Elia, Danieli na Nehemia.

Maombi

Ndani ya Agano Jipya tunaona Bwana wetu akisemezana na Baba yake mara nyingi kwa njia ya maombi. Aliomba mara saba ndani ya Luka, ndiyo Habari Njema ambayo inamwonyesha kama Mtu. Kwa maisha yake mazima Mwokozi aliomba kwa Baba yake. Luka aliandika maombi yake kwa wakati wa ubatizo wake (Luka 3:21), na wakati alipotia roho yake kwa mikono ya Mungu (Luka 23:46). Kuna mifano mingi mingine ya maombi ndani ya Matendo na Barua 21 za Agano Jipya.

Kielezo cha maombi

Bwana Yesu Kristo alitupa sisi kielezo kikamilifu ndani ya Matayo 6:9-13. Hakukusudi kwa sisi kutumia maneno ya ombi hili tena na tena, na hatusomi ya kwamba Wakristo kwa wakati wa mwanzo wa Kansa walifanya hivi. Lakini Bwana alikusudi ombi hili kuwa kielezo kutufundisha maneno makubwa:

1. Wakati tunapoomba inatupasa kuanza na kuabudu (sh.9).
2. Sharti tuombee kazi ya Bwana mbele ya kujiombea wenyewe na mahitaji yetu; *"ufalme wako uje"* (sh.10).
3. Hata saa ya kuomba inatupasa kukubali jibu la Mungu kwa maombi haya, hata kama akichagua kutofanya neno ambalo tunaomba; "*Mapenzi yako yatimizwe"* (sh.10).

Mafundisho juu ya maombi

Wakristo wanaagizwa kuomba. Usikose kusoma mashairi haya: Matayo 7:7; 26:41; Yoane 16:24; Wafilipi 4:6; Yakobo 1:5.

Inatupasa kuomba WAKATI GANI? Kwa kila wakati. Inatupasa kudumu sana katika maombi, pasipo kuacha (Waefeso 6:18; Wakolosayi 4:2; 1 Watesalonika 5:17). Inatufariji sana kujua ya kwamba Mungu anasikia maombi yetu kila mara.

Inatupasa kuomba PAHALI GANI? Pahali pote, ona 1 Timoteo 2:8.

Inatupasa kuomba NAMNA GANI? Zamani Waisraeli walisimama mbali wakati Musa alipokaribia giza zito pahali Mungu alipokuwa (Kutoka 20:21). Nyuma, wakati Kristo alipokuwa duniani naye hajakufa bado msalabani, pazia hekaluni lilitenga watu na Mungu mtakatifu (Luka 1:10). Lakini pazia hili lilipasuliwa kwa vipande viwili wakati Kristo alipokufa na sasa waamini

hawahitaji kukaa mbali tena. Mungu anawaita kumkaribia (Waebrania 10:19-22). Sasa kila mwamini anaweza kukaribia Mungu Baba kwa njia ya Mwana wake na katika Roho Mtakatifu. Ona Waefeso 2:18. Mungu amekubali malipo ya Mwana wake kwa zambi na sasa tunaweza kukaribia kiti chake cha ufalme na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrana 4:16).

Tunaweza kuja na uhodari, lakini sharti tufike na unyenyekevu vilevile. Ni lazima kwetu kukumbuka ya kwamba Baba yetu ya mbinguni ni Mungu wa milele vilevile, na sharti wale ambao wanamkaribia wafanye hivi na heshima na woga (Zaburi 89:6-7), wakiwa wenye mikono safi na mioyo miupe (Zaburi 24:3-4).

Waroma 8:23, 26-27 yanaonyesha ya kwamba Roho Mtakatifu anajulisha Mungu mizigo na kuugua kwa mioyo yetu. Inatupasa kuacha Roho Mtakatifu *kutuongoza ndani ya maombi yetu* na sharti tuombe kila mara kwa *uwezo wa Roho Mtakatifu* (Waefeso 6:18; Yuda 20). Hivi si maombi ya kweli wakati mtu anaposoma tu ombi ambalo mtu mwingine aliandika.

Inatupasa kuomba *kwa jina la Kristo* (Yoane 14:13-14). Si kusema tu kwa mwisho wa maombi yetu "kwa jina la Kristo, Amina." Wakati tunapoomba kwa jina lake, tunaomba kwa amri na ruhusa yake. Lakini neno hili linawezekana tu kama maombi yetu yakipatana na mapenzi yake yanayofunuliwa ndani ya Neno la Mungu (1 Yoane 5:14-15). Tukumbuke vilevile ya kwamba Mungu atajibu maombi yetu tu kama tukimtii ndani ya maisha yetu ya kila siku (Yoane 15:7). Haifai tuombe tu bule bila kutaja wazi maneno tunayotaka Mungu kutufanyia au kutuwezesha kufanya. Kwa mfano waamini katika Yerusalema waliombea Petro wakati alipokuwa gerezani (Matendo 12:5). Sharti tudumu katika maombi wakati Mungu asipotujibu mara moja (Luka 11:5-10; 18:1-8).

Uwezo wa maombi

Yakobo anatuambia ya kwamba maombi ya mtu mwenye haki yana faida kubwa (5:16). Maombi yenyewe hayana uwezo na hayawezi kugeuza maneno, lakini wakati tunapoomba Roho Mtakatifu anaweza kufanya maneno tunayoomba. Elia ni mfano mzuri wa neno hili (Yakobo 5:17-18).

Maombi

Maombi yasiyopata jibu

Tunajua Mungu hajibu maombi yetu yote, na ya kuwa hajibu kila mara namna tunavyotaka. Lakini sharti tukumbuke ya kwamba labda Mungu atajibu maombi haya nyuma kama asipofanya hivi mara moja. Mungu anatupenda na atafanya tu maneno yale yaliyo na faida na baraka kubwa zaidi kwetu.

Mungu hatajibu maombi ya mwamini—

1) kama asipokiri bado mbele ya Mungu zambi aliyofanya (Isaya 59:1-2; Zaburi 66:18; 1 Yoane 3:20-22);
2) kama akikataa kusamehe watu wengine (Marko 11:25-26);
3) kama akiomba maneno kwa faida yake mwenyewe tu (Yakobo 4:3);
4) kama asipokaa vizuri na mke wake (1 Petro 3:7);
5) kama akiomba bila kuamini ya kwamba Mungu anaweza kujibu maombi yake (Yakobo 1:6-7).

- 8 -

Kanisa na Biblia

Watu wengi hawajui kabisa kama maana ya neno hili "kanisa" ni nini. Wanasema juu ya Kanisa Protestant au Kanisa Katoliki, au sehemu mbalimbali za Kanisa Protestant, kama Kanisa Methodiste au Kanisa Baptiste. Watu wengine wanafikili kanisa ni jengo pahali Wakristo wanapokutana. Biblia haitumii neno hili "kanisa" na maana hizi. Tuone kama Kitabu cha Mungu kinafundisha nini juu ya kanisa.

Neno kwa "kanisa" ndani ya Kiyunani ni eklesia, maana yake *kusanyiko la watu walioitwa kutoka katikati ya watu wengine*. Ndani ya Biblia Kanisa ndilo watu wanaoitwa toka dunia kufuata Bwana Yesu Kristo. Dunia imekataa Kristo na inapasa Kanisa kumshuhudia. Hivi neno hili "kanisa" haliko kamwe wasioamini au jengo.

Ndani ya Agano Jipya neno hili *kanisa* linatumiwa kwa njia mbili:

1) Waamini wote duniani ni Kanisa linaloitwa vilevile "Mwili wa Kristo" (Wakolosayi 1:18,24). (Tutaliandika na "K" kubwa.)
2) Waamini wa pahali fulani wanaitwa kanisa la pahali pale. (Tutaliandika na "k" ndogo.)

KANISA KATIKA DUNIA NZIMA

Tuwaze juu ya mwanzo wa Kanisa, watu gani wanaweza kuwa ndani ya Kanisa, na kama Kanisa litakuwa namna gani kwa wakati wa kuja.

Mwanzo wa Kanisa

Kanisa ni Mwili wa Kristo. Halikuwa kwa wakati wa Agano la Kale. Lilianzwa wakati Roho Mtakatifu alipokuja toka mbinguni kukaa ndani ya waamini siku ya Pentekote. Mungu alikusudi tangu zamani kujenga Kanisa lake, lakini shauri hili lilikuwa siri

katika eoni zinazopita (Waefeso 3:9-11; Wakolosayi 1:24-26). Mtu wa kwanza aliyepasha watu habari za Kanisa alikuwa Bwana wetu, ndani ya Matayo 16:18. Alisema, "Nitajenga kanisa langu." Maneno haya yanaonyesha wazi ya kwamba kwa wakati ule Kanisa halikuwa kwanza. Shairi hili na Matayo 18:17 ndiyo mashairi ya pekee ndani ya vitabu vine vya Habari Njema yanayotaja Kanisa.

Ndani ya sura 2 ya Matendo tunasoma juu ya kuja kwa Roho Mtakatifu wakati Mungu alipokwisha kutukuza Bwana Yesu Kristo kwa mkono wake wa kuume (sh.33). Mwili wa Kristo haukuwa duniani wakati Kichwa (ndiye Bwana mwenyewe) asipokuwa bado mbinguni. Basi Kristo hakufika kule kama Kichwa kufika saa alipofufuliwa toka wafu na kurudia mbingu.

Neno hili linahakikisha ya kwamba Kanisa lilianzwa siku ya Pentekote. Soma Waefeso 1:20-23.

Watu gani ni ndani ya Kanisa?

Kanisa si chama au serikali. Ni mwili ulio hai wenye viungo wengi walio wote waamini wa kweli. Kweli hii inaelezwa wazi ndani ya barua kwa Waefeso pahali Kanisa linaposawanishwa na mwili (1:23) na bibi-arusi (5:25). Linasawanishwa na jengo vilevile, ndani ya 2:20. Mwili unatufikilisha *uzima*; jengo ndilo *pahali pa kupanga*, na bibi-arusi anatukumbusha *mapendo*. Roho Mtakatifu alianza Kanisa (1 Wakorinto 12:13), naye analifunganisha pamoja (Waefeso 4:3,13). Kristo ni Kichwa cha Kanisa (Wakolosayi 1:18), na Neno la Mungu linafundisha watu wa Kanisa kama ikiwapasa kufanya nini. Barua za Paulo ndani ya Agano Jipya zina mafundisho makubwa mengi kwa Kanisa.

Nini litapata Kanisa kwa wakati wa kuja?

Mungu anakusudi kwa Kanisa kushiriki ndani ya utukufu wa milele wa Kristo na Kristo atajiletea mwenyewe Kanisa la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi (Waefeso 5:27). Neno hili litafanyikana kwa arusi ya Mwana-Kondoo, ndio wakati wa furaha kubwa kwa wote walio mbinguni. Kisha Bwana Yesu Kristo, Bwana-Arusi, ataona matunda ya taabu yake yote na atatulia (Isaya 53:11; Ufunuo 19:7-9).

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

KANISA LA PAHALI FULANI

Neno hili "kanisa" linatumiwa vilevile kwa waamini wa pahali pamoja. Maandiko Matakatifu hayatumii neno hili kamwe kwa waamini wa inchi nzima, kama "Kanisa la Congo". Ndiyo, tunasoma juu ya *makanisa* ya Galatia (Wagalatia 1:2); makanisa ya Mungu katika Yudea (1 Watesalonika 2:14); si kanisa la Galatia au Yudea. Ona 1 Wakorinto 11:16; Waroma 16:4,16.

Makanisa haya si sehemu za chama moja ambayo inawaagiza nini inawapasa kufanya, lakini makanisa yote wana Kichwa mmoja, ndiye Bwana Yesu Kristo. Makanisa yote wanaongozwa na Roho Mtakatifu, nayo yote wana kazi moja, ndiyo kushuhudia Kristo na kutangaza kweli ya Mungu kwa watu wengine, na kungaa kama taa katikati ya watu wa dunia hii (Wafilipi 2:15-16).

Watu gani ni ndani ya kanisa la pahali fulani?

Kanisa kwa Filipi lilikuwa watu wote waliokuwa wameamini Bwana Yesu Kristo, pamoja na waangalizi wa kanisa na watumishi (Wafilipi 1:1). Shairi hili na mashairi mengine yanaonyesha wazi ya kwamba kanisa la Mungu ni waamini wote wa kweli wa pahali pale. Kwa mwanzo waamini wote wa pahali fulani walishiriki na fungu la pekee la waamini kwa pahali pale na tunasoma juu ya *kanisa la Mungu lililo katika Korinto*, vivi hivi. Si hivi kwa wakati wa sasa. Leo waamini wengi wa kweli wanafungana na sehemu mbalimbali za kanisa Protestant zenye mafundisho mbalimbali juu ya maneno kama kuabudu, ubatizo na mengine. Hata hivi waamini wa kweli wote wa pahali fulani ni *kanisa la Mungu* katika pahali pale. Hata waamini wachache wanaokutana pamoja nyumbani mwa mmoja wao wanaweza kuitwa "kanisa". Soma 1 Wakorinto 16:19; Wakolosayi 4:15. Ona ya kwamba ndani ya mashairi haya haliitwi *kanisa la Mungu*, lakini kanisa *ndani ya nyumba.*

Kanisa la pahali po pote wanazunguka Bwana Yesu mwenyewe wakati wanapokutana. Yeye ni katikati yao, hata wakati watu wawili au watatu tu wanapokutana kwa jina lake (Matayo 18:20).

Mwili wa Kristo ndio waamini wote wa kweli. Sisi ni viungo vya Mwili wake. Karamu ya Ukumbusho ni mfano wa umoja huu (1 Wakorinto 10:16-17). Roho Mtakatifu anaweza kuongoza watu

wa kanisa la pahali fulani ndani ya kuabudu kwao na kutumika nao kufundisha Neno la Mungu.

Ni kazi ya wazee kuongoza maneno ya kanisa kwa utaratibu na kuhukumu mwamini ye yote anayeanguka na kufanya zambi.

Kusudi la kanisa kwa pahali fulani

Kinara cha zahabu ndani ya Ufunuo 1:20 ni mfano wa kanisa la pahali fulani. Zahabu inasema juu ya haki ya Mungu na kinara kinatukumbusha ya kwamba kusudi la kweli la kanisa lo lote ni kuwa nuru na kushuhudia Kristo ndani ya dunia hii ya zambi wakati yeye asipokuwa hapa. Kusudi la kanisa si kugeuza dunia kuwa pahali pazuri kupita kwa watu kukaa ndani yake, lakini ni kutangazia watu wa dunia habari za Bwana Yesu Kristo na kazi aliyofanya juu ya msalaba ili watu wote waweze kuokolewa. Hivi inapasa kanisa kuwa na ushuhuda kwa watu wa pahali pale, na vilevile kutuma Wakristo wengine kupeleka habari za wokovu kwa watu wa inchi nyingine.

Uwezo wa kanisa la pahali fulani

Kanisa la kila pahali linahitaji uwezo wa Roho Mtakatifu anayesaidia kila mwamini kuabudu Mungu (Wafilipi 3:3), na kushuhudia Kristo (Matendo 4:31; 13:2; 1 Wakorinto 3:16). Ndugu za kanisa la pahali fulani wanahitaji Roho Mtakatifu kuwasaidia kushikamana na utaratibu wa kanisa ambao Mungu alionyesha ndani ya Kitabu chake, na kushuhudia Kristo.

Soma tena mafundisho ya sura hii juu ya kanisa la pahali fulani na Kanisa zima duniani. Umeyafahamu vizuri? Halafu soma mashairi yanayofuata na chagua kama kila shairi likisema juu ya kanisa kwa pahali fulani au juu ya Kanisa zima duniani. Andika majibu yako juu ya mistari kwa upande wa kuume wa kila shairi.

1 Wakorinto 1:2 _____

Waefeso 3:10 _____

Wakolosayi 4:15 _____

1 Wakorinto 14:23 _____

Wakolosayi 1:18 _____

- 9 -

Makuhani wanaoabudu na kutumikia

MAKUHANI WALIO WAKRISTO

Waisraeli katika Agano la Kale walikuwa taifa la askari (Hesabu 1:3).

Moja la makabila yao walikuwa kabila la watenda kazi, ndio Walawi (Hesabu 1:50).

Moja ya jamaa za kabila lile walikuwa jamaa ya waabudaji. Walikuwa Haruni na wana wake, ndio makuhani (Kutoka 28:1; Hesabu 3:3).

Makuhani hawa walikuwa namna nyingine na watu wengine kwa sababu walisimamisha hema zao kwa pahali palipoagizwa na Mungu na kwa sababu mavazi yao yalikuwa namna nyingine na mavazi ya watu wengine. Walikula vyakula fulani ambavyo watu wengine hawakuweza kula. Mungu aliwapendelea kwa maneno mengine na iliwapasa kufanya kazi ambayo watu wengine hawakuwa na ruhusa kufanya. Ona Kutoka 28; Walawi 7:6-10; Hesabu 8:2; 10:8-11.

Makuhani tu walikuwa na ruhusa kuingia Pahali Patakatifu Sana hekaluni mbele ya Mungu mtakatifu. Waliingia na kufika mbele ya Mungu kwa ajili ya watu, na walitoka tena karibu na watu kwa ajili ya Mungu. Walisimama katikati ya Mungu na watu.

Haruni alikuwa kuhani mkubwa wa pekee; wana wake walikuwa makuhani tu. Makuhani tu walitoa zabihu juu ya mazabahu nao peke yao walikuwa na ruhusa kuingia pahali patakatifu hekaluni. Makuhani tu waliweza kusema kama mtu alikuwa na ukoma au kama alikuwa ameponyeshwa toka ugonjwa ule mbaya.

Makuhani wa Agano la Kale ni mfano wa makuhani ya kweli kwa wakati wa sasa. Makuhani hawa ni wanani? Waamini wote wa kweli ni makuhani. Usikose kusoma 1 Petro 2:5, 9 na Ufunuo

Makuhani wanaoabudu na kutumikia

1:5-6; 5:10. Haya ndiyo mashairi yote yanayofundisha juu ya neno hili. Makuhani katika Agano la Kale hawakuwa makuhani kwa sababu wao wenyewe walichagua kuwa makuhani, au kwa sababu walijifunza sana, lakini walikuwa makuhani kwa sababu walizaliwa ndani ya jamaa ya Haruni. Hakuna mtu mwingine aliyeweza kuwa kuhani (Ezra 2:62).

Kwa wakati wa sasa vilevile hakuna mtu aliye kuhani kwa sababu anachagua kuwa kuhani au kwa sababu ya kujifunza sana, lakini anageuka kuhani wakati anapoamini Kristo na kuzaliwa tena kwa njia ya Roho Mtakatifu. Ndani ya 1 Wakorinto 12 na Waefeso 4 tunaona zawadi nyingi Roho Mtakatifu anazotolea Kanisa, lakini hutaona zawadi ya kuhani katikati yao. Kazi ya kuhani si zawadi kwa sababu waamini wote wa kweli ni makuhani. Kuna watu wengine kwa wakati wa sasa ambao wanajiita makuhani lakini wao si makuhani wa kweli. Watu wa jamaa ya Haruni tu walikuwa makuhani katikati ya Wayuda nao walitumika hapa duniani ndani ya hekalu la dunia. Walikuwa mfano wa makuhani wa wakati wa sasa. Lakini leo watu wote walio ndani ya jamaa ya Mungu ni makuhani. [Inatupasa kuabudu Baba namna gani? Yoane 4:24 _____]

Kama kuhani mtakatifu Mkristo anaweza kutolea Mungu zabihu za roho (1 Petro 2:5). Akiwa kuhani wa Mfalme anatangaza uzuri wa Mungu kwa watu (1 Petro 2:9). Kwa mfano Paulo na Sila walitenda kama makuhani watakatifu katika Matendo 16:25 na kama makuhani wa Mfalme ndani ya shairi 31 la sura ile ile. Mfano mwingine wa neno hili ni ndani ya Waebrania 13. Shairi 15 linatupasha juu ya kazi ya makuhani watakatifu na shairi 16 juu ya kazi ya makuhani ya Mfalme.

Kwa wakati wa sasa makuhani wengine wanavaa mavazi namna nyingine na wana ruhusa na kazi ndani ya makanisa yao zinazokatazwa kwa watu wengine. Makuhani hawa wanaiga ukuhani wa Wayuda. Hakuna makuhani namna hii katikati ya Wakristo wa kweli leo kwa sababu Wakristo wote ni makuhani nao wote wana ruhusa sawasawa na inawapasa wote kuabudu Mungu. Haruni na wana wake ni mfano wa Bwana Yesu Kristo, Kuhani Mkubwa, na watu wake wote ambao aliwanunua na damu yake ya damani.

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

WAABUDAJI

Tuwaze sasa juu ya maana ya kuabudu, pahali gani inapotupasa kuabudu, na uwezo kwa kuabudu.

Maana ya kuabudu

Mtu anaabudu wakati moyo wake unapofurika na sifa saa anapowaza juu ya Mungu na namna anavyofunuliwa ndani ya Kristo. Anaabudu Mungu Baba na Mungu Mwana kwa sababu amefunguliwa toka utumwa wa zambi kwa njia ya zabihu ya bei kubwa ya Kristo. Makuhani wa kweli tu (wa namna ya mafundisho ya Agano Jipya) wanaweza kuabudu.

Vizuri tufahamu ya kwamba kuabudu na kufundisha Neno la Mungu ni maneno mbalimbali. Kuabudu kwetu kuna*panda kwa Mungu,* lakini wale wanaofundisha Neno la Mungu wanafanya hivi kusaidia watu, hivi mafundisho yao *yanatoka Mungu* kwa watu. Mwamini anafundisha watu wengine kweli yeye mwenyewe alizopokea toka Mungu Baba, kwa njia ya Mungu Mwana, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Lakini wakati anapoabudu, kuabudu kwake kunapanda juu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, kwa njia ya Mwana kufikia Baba.

Pahali inapotupasa kuabudu

Waisraeli waliabudu Mungu ndani ya jengo hapa duniani, na walitumia vitu mbalimbali kwa zabihu zao. Mkristo hahitaji kuwa ndani ya nyumba fulani kwa kuabudu Mungu lakini pahali po pote alipo anaweza kufika mara moja mbele ya Mungu. Soma Waebrania 10:19-22 polepole. Makuhani wa zamani waliweza kutolea Mungu zabihu nasi tunaweza kufanya vivyo hivyo. Sharti tujitoe wenyewe kwa Mungu (Waroma 12:1). Tunaweza kusifu Mungu vilevile na sauti zetu na kutoa mali kusaidia watu wengine (Waebrania 13:15-16).

Uwezo kwa kuabudu

Tunaweza kuabudu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tu (Wafilipi 3:3). Roho Mtakatifu anapenda sana kuondosha mafikili yetu toka maneno yetu wenyewe na kuyakokota juu ya utukufu wa Mungu na Kristo.

Makuhani wanaoabudu na kutumikia

WATUMISHI WA MUNGU KANISANI

Ni lazima kwa waamini kulishwa na Neno la Mungu waweze kutembea karibu na Bwana. Kristo ni Kichwa cha Kanisa, naye peke yake analikulisha na kulilinda (Waefeso 5:29). Anafanya hivi kwa njia ya Roho Mtakatifu na kwa njia ya kuwapa waamini wengine zawadi ya kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu au kulinda waamini kwa njia nyingine. Waamini wote ni makuhani kwa sababu wamezaliwa tena, lakini si waamini wote walio na zawadi ya kufundisha au kuhubiri.

Ndani ya Waefeso 4:11-13 tunaona zawadi Wakristo wana-zopewa kwa wakati wa sasa. Kuna wahubiri wa Habari Njema, wachungaji, na walimu. (Hakuna mitume na manabii kwa wakati wa sasa, lakini tuna vitabu ambavyo waliandika.)

Mhubiri wa Habari Njema anapeleka Habari Njema ya wokovu kwa wenye zambi pahali pote duniani. Filipo alikuwa mhubiri wa Habari Njema (Matendo 21:8).

Mchungaji analinda watu waliookolewa. Anawafikisha kwa kanisa la kijiji chao na kuwaongoza kufuata njia ya Mungu.

Hatusomi hata mara moja ndani ya Agano Jipya ya kwamba kulikuwa na mchungaji mmoja tu kulinda kanisa la pahali fulani. Tunaona tena na tena ya kwamba kwa wakati Agano Jipya lilipoandikwa makanisa yalikuwa na wachungaji zaidi ya mmoja kila mara. Wachungaji hawa wanachaguliwa na Bwana mwe-nyewe, si na Wakristo wengine, nao wanalinda watu wa Mungu na upole na mapendo. Ona 1 Watesalonika 2:7,11.

Mwalimu anaeleza Neno la Mungu kwa utaratibu na kwa njia hii anapatisha waamini nguvu katika imani.

Mzee (anaitwa mwangalizi vilevile) ni mtu anayetembea karibu na Bwana na kujuana naye sana. Kazi yake ni kulinda kanisa (1 Timoteo 3:5); kulisha waamini na Neno la Mungu (1 Petro 5:2); na kuwasimamisha (Matendo 20:28-30). Wazee wanatumika ndani ya kanisa la pahali wanapokaa na wengine wana zawadi ya kufundisha au kuhubiri vilevile mbele ya watu (1 Timoteo 5:17). Ndani ya kila kanisa kwa wakati Agano Jipya lilipoandikwa kulikuwa na wazee kupita mmoja (Matendo 14:23; Tito 1:5).

- 10 -

Utumishi wetu kwa Bwana

Sura hii ina mafundisho makubwa kwa kila mwamini anayependa Bwana na anayetaka kumpendeza. Sharti tufahamu mafundisho haya, na zaidi ya ile ni sharti kwetu kuyatii.

Mungu anampa kila Mkristo kazi kufanya kwa yeye. Ona Marko 13:34. Kwa wakati wa sasa watu wengi wanafikili ya kwamba wakubwa wa kanisa na wahubiri tu wanaweza kufanya kazi ya Mungu lakini haya si mafundisho ya Biblia. Neno la Mungu linasema Kanisa ni kama mwili wa mtu ulio na viungo mbalimbali vingi wanaofanya kazi pamoja. Kichwa kinaongoza viungo, ndivyo mikono, miguu, masikio, ulimi na viungo vyote vingine. Kila kiungo kina kazi kubwa iliyo mbali na kazi ya kila kiungu kingine; na kila kiungo kinasaidia mwili mzima. Viungo vya mwili havipigani, lakini vinasaidia viungo vyote vingine. Mwili unahitaji kila kiungo, na viungo mbalimbali vya mwili vinategemeana. Mguu wa kuume unahitaji mguu wa kushoto, vidole vinahitajiana. Ni vivyo hivyo na viungo vyote vingine.

Soma mashairi haya polepole: 1 Wakorinto 12:12-32; Waroma 12:4-8; Waefeso 1:19-23. Mashairi haya yanatufundisha maneno makubwa matatu:

1. Kristo mbinguni ni Kichwa cha Kanisa.
2. Mwili wa Kristo duniani ndio waamini wote wa kweli.
3. Kichwa anampa kila mwamini kazi fulani ambayo inampasa kufanya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Mungu hataki kwa vingine vya viungo ndani ya mwili wa Kristo kukaa bule.

Sasa tufikili juu ya maneno haya:

Utumishi wetu kwa Bwana

1. Bwana ambaye tukamtumikia
2. Sababu kwa kazi yetu
3. Kristo ataangalia kazi yetu

Bwana ambaye tunatumikia

Agano Jipya linafundisha waziwazi ya kwamba Kristo ni Mwokozi na Bwana wetu. Yeye ni **Mwokozi** wetu ambaye alituokoa toka azabu tuliyostahili kupata kwa sababu ya zambi zetu. Kristo ni **Bwana** wetu aliye na amri kutuagiza nini inatupasa kufanya. Watu wengi wanapokea Kristo kuwa **Mwokozi** wao ili wasifikie ziwa la moto, lakini wengine hawafahamu ya kwamba yeye ni **Bwana** wao vilevile. Watu wengi ni wadanganyifu ambao wanamwita "Bwana" lakini hawafanyi maneno ambayo anawaagiza kufanya. Saa ile tu tunapofahamu ya kwamba Kristo ni Bwana wa maisha yetu tutaweza kumtumikia vizuri. Mtume Paulo alijiita mtumwa wa Yesu Kristo (Waroma 1:1), na alitaka kufanya mapenzi yake tu ndani ya maneno yote.

Soma mashairi haya yanayofundisha wazi kabisa ya kwamba Yesu Kristo ni **Bwana**: Luka 2:11; Matendo 2:36; Waroma 10:9; Wakolosayi 2:6; 1 Petro 3:15. Ndani ya shairi gani unasoma ya kwamba

Kristo ni Bwana? _____

Yesu ni Bwana? _____

Kristo Yesu ni Bwana? _____

Sababu kwa utumishi wetu

Kila mara tuna sababu kwa neno lo lote ambalo tunafanya. Sababu hii ni neno kubwa kupita tendo lenyewe. Mungu anaona yote yaliyo mioyoni mwetu, naye anajua kama tukimtumikia kwa kumpendeza na kumtukuza **yeye** au kwa sababu tunataka watu waweze kutusifu **sisi**. Bwana Yesu Kristo alihukumu Wafarisayo kwa sababu walitenda sawasawa walitaka kutumikia Mungu lakini kabisa kabisa walitaka watu kuwasifu. Matendo yao yalikuwa mazuri, lakini waliyafanya na kusudi baya.

Mungu anaahidi kumpa zawabu kila mtu ambaye anasaidia Mkristo na maji ya kunywa (Marko 9:41). Kopo ya maji ni kitu

kidogo tu lakini mtu yule anaileta kwa sababu anataka kuonyesha mapendo yake kwa Bwana. Kusudi lake ni jema na hili ndilo neno kubwa.

Tunaona kweli hii ndani ya maisha ya Daudi vilevile (2 Mambo 6:8-9). Daudi alitaka kujengea Mungu nyumba kwa sababu alipenda Mungu na alitaka kumheshimu. Mungu hakumruhusu kufanya hivi, lakini alimsifu kwa sababu ali**taka** kufanya neno hili.

Ni sharti kwa sisi sote kutumikia Mungu, lakini inatupasa kujiuliza vilevile **kwa nini** tunamtumikia. Lazima tufanye maneno yote kwa utukufu wa Mungu tu (1 Wakorinto 10:31).

Bwana tu anajua mawazo yetu na kwa sababu gani tunamtumikia na haifai kwetu kujaribu kufahamu na kuhukumu makusudi ya watu wengine (1 Wakorinto 4:5). Lakini kwa wakati wa kuja Bwana atapima kazi yetu na kwa sababu gani tuliifanya.

Kristo ataangalia utumishi wetu

Haifai kwetu kuhukumu utumishi wa watu wengine. Bwana Yesu atafanya hivi wakati atakapofunua wazi siri na makusudi ya mioyo ya watu. Itapasa Wakristo wote kusimama mbele ya Kristo kwa kuhukumiwa naye (2 Wakorinto 5:10). Kwa wakati ule kila Mkristo atapokea sifa yake toka Mungu kwa kipimo anachostahili (1 Wakorinto 4:5).

Bwana Yesu alilipa bei kwa **zambi** zangu wakati alipokufa juu ya msalaba na Mungu hatanihukumu **mimi** juu ya zambi hizi kamwe. Lakini kwa wakati wa kuja Bwana atapima utumishi wangu kwa yeye. Hatafanya hivi kuona kama nikistahili kuokolewa au sivyo, lakini kama nikistahili kupokea zawabu.

Ni Bwana atakayesema kama tutapata zawabu na kama zawabu hii itakuwa zawabu ya kipimo gani. Neno kubwa si kipimo cha kazi tunachofanya kwa Bwana, lakini namna ya kazi yenyewe. Siku ile *namna* ya kazi ya kila mtu itajaribiwa kwa moto. Kama ikionekana kuwa njema mtu yule atapokea zawabu (1 Wakorinto 3:13-14). Soma vilevile Waebrania 10:35; 11:26; 2 Yoane 8; Ufunuo 22:12.

Mbele ya hukumu hii Bwana atapeleka Kanisa mbinguni.

- 11 -

Bwana atakuja tena

Kurudi kwa Bwana Yesu Kristo kunatajwa mara 318 ndani ya sura 260 za Agano Jipya, au mara moja ndani ya karibu mashairi 25. Mtu wa kwanza aliyehubiri juu ya kurudi kwa Bwana alikuwa Enoka, mzao wa saba wa Adamu (Mwanzo 5:21; Yuda 14). Masemo ya mwisho ya Bwana Yesu Kristo ndani ya Agano Jipya yalikuwa juu ya kurudi kwake (Ufunuo 22:20). Karibu vitabu 27 vyote vya Agano Jipya vinataja kurudi kwa Bwana. Hivi tunafahamu ya kwamba ni neno kubwa sana.

Bwana Yesu Kristo atakuja tena yeye mwenyewe mbele ya kuanza kutawala juu ya dunia kwa miaka 1.000.

Agano Jipya lina sehemu ine: vitabu vya Habari Njema, Matendo ya Mitume, Barua, na Ufunuo. Tusome mashairi ndani ya sehemu hizi zote ine juu ya kurudi kwa Bwana.

Kristo aliahidi kurudi

Aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba atakwenda kuwatengenezea pahali, kisha atarudi tena na kuwapeleka kwake (Yoane 14:2-3). Alitoa ahadi hii kuwafariji mangaribi iliyotangulia kufa kwake. Watu wengine wanafikili ahadi hii ilitimizwa siku ya Pentekote; wengine wanasema Bwana anakuja kwa kila mwamini saa ya kufa kwake. Tuulize basi, "Tunaweza kujua namna gani ya kwamba Kristo hakusema juu ya Pentekote?" Tunafahamu ya kwamba hakuwaza juu ya siku ya Pentekote kwa sababu zaidi ya mashairi yanayopasha juu ya kurudi kwake yaliandikwa *nyuma* ya Pentekote. Soma Matendo 3:20 na 1 Wakorinto 1:7 na jibu maulizo haya:

1. Nani atatuma Yesu tena hapa duniani? _____
2. Nani atafunuliwa? _____

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Bwana hakuwaza juu ya mauti vilevile wakati aliposema juu ya kurudi kwake. Kuja kwake ni mbalimbali kabisa na mauti. Kuja kwa Kristo kutageuza maneno yote mauti inayokwisha kutendea miili ya watu wa Mungu tangu miaka 6.000!

Ni lazima kwa Bwana wetu kurudi yeye mwenyewe. Aliahidi kufanya hivi na hawezi kuvunja ahadi yake.

Yule atakayekuja tena

Tufungue sasa kitabu cha Matendo, kitabu cha pekee cha historia ndani ya Agano Jipya. Ndani ya mashairi 9-11 ya sura 1 tunasoma juu ya mmoja atakayekuja tena. Bwana Yesu atarudi namna alivyokwenda mbinguni. Isaka alitoka kukutana na bibi arusi wake, ndiye Rebeka (Mwanzo 24:63), na Bwana Yesu atakuja yeye mwenyewe kwa Kanisa lake. Hili ndilo neno ambalo Kanisa linatazamia, tumaini lake kubwa (Tito 2:13).

Kwa nini Kristo atakuja tena

Kuna sababu tatu:

1. Kuonyesha ya kwamba maneno aliyosema ni kweli.
2. Kupeleka waamini mbinguni.
3. Kutawala juu ya dunia.

1. **Kuonyesha ya kwamba maneno aliyosema ni kweli.** Wakati Bwana Yesu aliposimama mbele ya kuhani mkubwa kwa kuhukumiwa kuhani alimwapiza na Bwana alisema yeye ni kweli Mwana wa Mungu, ya kwamba ataketi kwa mkono wa kuume wa Mungu na ya kwamba atakuja tena na mawingu ya mbingu (Matayo 26:64). Alisema maneno haya kupita mara moja wakati alipokuwa duniani na atakuja tena kuonyesha ya kwamba alisema kweli.

2. **Kupeleka waamini mbinguni**, waamini wa wakati wa Agano la Kale na wale wa muda huu wa Kanisa. Unaweza kuona habari nyingi juu ya neno hili ndani ya 1 Wakorinto 15:51-58; Wafilipi 3:20-21, na 1 Watesalonika 4:13-18. Usikose kusoma mashairi haya polepole kwani yanaeleza ahadi ya Mwokozi ndani ya Yoane 14. Kuja kwake kutakuwa gafula naye atakusanya watu wake mwenyewe kwenda pamoja naye. Watu wengine wataachwa hapa duniani.

Bwana atakuja tena

3. **Kutawala dunia.** Kuja tena kwa Kristo kutakuwa na sehemu mbili. Atakuja kwanza kama kwa siri na nyuma atakuja wazi mbele ya watu wote.

Kuja kwake hapa duniani mara ya kwanza kulikuwa na sehemu mbili vilevile, kwanza kwa siri, kisha mbele ya watu wote. Alifika kwanza kwa Betelehemu na alikaribishwa na wachungaji na waakili na watu wachache wengine. Nyuma alitokea waziwazi mbele ya watu wote wakati alipoingia Yerusalema kama Mfalme na elfu za watu walimwona (Matayo 21:1-9).

Kwa sehemu ya kwanza ya kuja kwake mara ya pili watakatifu wote waliokufa watafufuliwa, na watakatifu wote walio hai watageuzwa. Bwana atakutana nao katika mawingu na kuwapeleka mbinguni pamoja naye (1 Watesalonika 4:17). Kwa wakati wa sehemu ya pili ya kuja kwake hatafikia *hewa* tu, lakini *dunia*, na atasimama juu ya Mlima wa Mizeituni (Zekaria 14:4).

Siku moja Bwana Yesu na wanafunzi wake walisimama juu ya Mlima wa Mizeituni naye aliwaambia ya kwamba atakuja tena katika mawingu ya mbingu pamoja na malaika wote (Matayo 24:30; 25:31; 1 Watesalonika 3:13). Neno hili litatokea kwa mwisho wa Mateso Makubwa. Watawala waovu wa dunia watalazimishwa kuacha kutesa fungu dogo la waamini Wayuda kwa sababu Kristo ataokoa watu wake.

Halafu Kristo atahukumu mataifa yote ya dunia (Matayo 25:31-46). Watu wote walioasi Mungu wataazibiwa kwa milele, pamoja na Shetani, kiongozi wao. Kisha Kristo atasimamisha ufalme wake duniani utakaoendelea kwa miaka 1.000 (Ufunuo 20:1-6). Soma vilevile Isaya 2:1-5; 4:2-6; 11:1-9; 35:1-10; Amosi 9:13-15; Mika 4:3. Mashairi haya yanatufundisha maneno mengine juu ya muda huu wa miaka 1.000.

Namna gani tunaweza kukaa tayari kwa kuja kwa Kristo?

Inatupasa kukumbuka saa zote ya kwamba Bwana anaweza kutokea sasahivi. Neno hili litatusaidia kuishi maisha safi na matakatifu (1 Yoane 3:3). Tunatumaini ya kwamba kuja kwake ni karibu na tumaini hili linaongeza saburi yetu (Yakobo 5:7-8), na linatusaidia kuangalia pamoja na maombi (1 Petro 4:7).

MAZIWA KWA WAAMINI WA SASA

Linatusaidia kutumikia Bwana na kustahili kupokea taji (2 Timoteo 4:5-8), linajaza mioyo yetu na salama (Wafilipi 4:5-7), na kutusukuma kuhubiri Habari Njema ya Kristo (2 Timoteo 4:1-2). Sharti tuzidi saa zote kutenda kazi ya Bwana, kwani atakuja nyuma kidogo kuangalia kazi yetu na kuona kama tukistahili kupokea taji (1 Wakorinto 15:58).

- 12 -

Taji na Zawabu

Agano Jipya linatupasha juu ya hukumu kubwa ine na ni lazima kwetu kufahamu tofauti katikati yao:

1. Hukumu ya zambi za mwenye zambi msalabani.
2. Hukumu ya kazi za mwamini kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo.
3. Hukumu ya mataifa walio duniani wakati Kristo atakaporudi na utukufu (Matayo 25:31-46).
4. Hukumu ya waovu waliokwisha kufa kwa Kiti Kikubwa Cheupe (Ufunuo 20:11-15).

Ya kwanza ya hukumu hizi inakwisha kutokea wakati Mwokozi alipokufa msalabani lakini hukumu tatu nyingine ni kwanza mbele yetu. Hukumu ya pili itatokea mara moja wakati Bwana atakapokwisha kupeleka Kanisa mbinguni. Hukumu ya tatu itakuwa saa ndogo tu mbele ya mwanzo wa utawala wa Kristo kwa miaka 1000, na hukumu ya ine kwa mwisho wa muda ule. Hakuna mwamini wa kweli atakayehukumiwa kwa Kiti Kikubwa Cheupe kwani Bwana Yesu Kristo amebeba hukumu kwa zambi zake wakati alipokufa juu ya msalaba (Yoane 5:24; Waroma 8:1).

Ndani ya Somo 10 tuliona ya kwamba matendo yetu na kazi zetu kwa Bwana zitahukumiwa kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo. Kwa wakati ule Bwana Yesu mwenyewe atatafuta maneno ya maisha ya kila Mkristo, namna gani alitumia saa, zawadi, nguvu na mali yake wakati alipokuwa duniani, na kama alifanya hivi kwa sababu gani. Soma 1 Wakorinto 3:10-15 polepole.

Kila Mkristo anatumia maisha yake kwa utukufu wa Mungu au kwa faida yake mwenyewe. Bwana ataangalia maneno yote tuliyofanya. Moto utateketeza maneno bule yaliyo kama miti na nyasi, lakini mambo mazuri ni kama zahabu, feza na mawe ya bei

kubwa na moto hauwezi kuyateketeza. Hivi Bwana ataharibu yote yasiyokuwa kwa utukufu wake. Waamini wengine wametumikia Bwana kwa miaka mingi; kazi yao itadumu milele. Wengine wamepoteza maisha yao; wataona kazi zao zote zikiteketezwa na kupotea, lakini wao wenyewe wataokolewa.

Tunajua kabisa ya kwamba Kristo atampa Mkristo zawabu kwa kila kazi anayokwisha kufanya kupendeza Bwana wake. Lakini kutakuwa na waamini wengine walioishi maisha yao kwa kujipendeza wenyewe tu, si kwa Bwana. Watakuwa na huzuni kubwa wakati watakapofahamu upumbavu wao. Wokovu wao hautawapotelea, lakini hawatapokea zawabu. Msingi wa wokovu wetu si matendo yetu wenyewe, lakini kazi Kristo aliyofanya kwa ajili yetu juu ya msalaba, lakini tutapokea zawabu tu kupatana na namna tulivyotumikia Bwana na kwa kusudi gani.

Mtu mmoja alieleza kweli hii kubwa kwa njia ya hadizi:

Baba mmoja alituma mwana wake kwa mji mwingine aweze kumfanyia kazi fulani kule. Alimpa mali ya kutosha kwa safari ya kwendea mji ule na kwa kurudi tena na alimfundisha waziwazi nini ilimpasa kufanya kule. Alimwonya vilevile kutumika na nguvu bila kupoteza saa kwa sababu ataweza kubaki kule kwa muda mfupi tu.

Kijana alifikia mji, akaanza mara moja kufanya kazi ambayo baba yake alimwagiza kufanya. Lakini nyuma kidogo alikutana na rafiki wengine, akakwenda na kuzungumuza pamoja nao, akasahau kabisa kazi ya baba yake. Gafula alikumbuka maneno ambayo ilimpasa kufanya, lakini saa ilikuwa imepita na sasa ilikuwa saa kwa kurudi kwake.

Alikuwa *tayari* kwa safari ya kurudi kwake? Ndiyo na sivyo! Alikuwa na mali ya kutosha kumwezesha kurudi kwake, ndiyo mali ambayo baba alimpa, lakini hakumaliza kazi yake. Wakati alipofika kwake, baba hakuweza kumsifu juu ya kazi aliyofanya. Hata hivi kijana alikuwa mwana wa baba yake tu na aliweza kukaa pamoja na ndugu zake nyumbani mwa baba.

Juu ya msalaba Bwana Yesu Kristo alilipa bei iliyohitajiwa kwa kila mwamini kuweza kwenda mbinguni. Wao wote wamehesabi-

wa haki naye na atashiriki utukufu wake pamoja nao (Waroma 8:30), lakini zawabu watakazopokea zitakuwa mbalimbali. Mungu atampa kila Mkristo zawabu kwa kipimo cha uzuri cha kazi aliyofanya (1 Wakorinto 3:8). Lakini wale wasiopokea zawabu ni wana wa Mungu tu hata hivi na watakaa mbinguni kwa milele.

Tuone maneno mane mengine juu ya Kiti cha Hukumu cha Kristo:

1. Bwana Yesu Kristo ata**angalia** maisha na kazi ya watumishi wake (Matayo 18:23; Luka 19:15).
2. Ata**onyesha wazi** uzuri au ubaya wa kazi ya kila mtu (1 Wakorinto 3:13; 2 Wakorinto 5:10).
3. Ata**sifu** watu wale waliokuwa watumishi wema na waaminifu (Matayo 25:21; 1 Wakorinto 4:5).
4. Ata**toa zawabu**. Biblia inatupasha juu ya taji mbalimbali tano:
   1) *taji ya haki,* kwa wale wanaopenda Bwana na wanaotazamia kuja kwake (2 Timoteo 4:8).
   2) *taji isiyoharibika*, kwa wale wanaotumikia Bwana na roho yao yote (1 Wakorinto 9:25).
   3) *taji ya uzima,* ndiyo zawabu ambayo Mungu atawapa waamini wale wanaokaa waaminifu kwa wakati wa mateso (Yakobo 1:12).
   4) *taji ya utukufu*, kwa viongozi walio mfano mzuri kwa Wakristo wengine (1 Petro 5:4).
   5) Paulo alisema juu ya waamini wengine ambao alisaidia na aliwaita *taji* yake (Wafilipi 4:1; 1 Watesalonika 2:19).

Bwana aliahidi kutupa sisi zawabu kama:

1) tukipanda haki kwa njia ya kusaidia watu wengine (Mezali 11:18);
2) tukisaidia watu wale wasioweza kutulipa (Luka 14:14);
3) tukiomba na bidii na kwa siri (Matayo 6:6);
4) tukisaidia Mkristo na maji ya kunywa (Marko 9:41);
5) tukipata mateso kwa sababu tuko watu wa Kristo (Luka 6:22-23)

6) tukipendeza Mungu nyumbani mwetu (Ruta 2:11-12);
7) tukiangalia nafsi zetu na zile za watu wengine (2 Yoane 8).

Tutapokea zawabu yetu pahali gani? Ona Matayo 5:12.

_____

Wadanganyifu watapokea zawabu yao wapi? Ona Matayo 6:2,5,16.

Basi tuna Mwokozi wa ajabu kabisa! Wakati tulipokuwa kwanza wenye zambi alituokoa kwa njia ya imani tu. Anatusaidia kufahamu Maandiko Matakatifu ili tuweze kujua kabisa ya kwamba tumeokolewa. Ametupa sisi tabia mpya ili tuweze kupendeza Mungu. Anatupa uwezo ili tuweze kuishi maisha ya kushinda. Ametutayarishia Karamu ya Ukumbusho ili tuweze kukaa kumkumbuka. Anatusaidia kujitenga na dunia na anajibu maombi yetu. Anatufundisha namna gani inatupasa kukutana pamoja kwa kumwabudu. Anatuheshimu sana kwa njia ya kuturuhusu kumtumikia na anaahidi kutupa sisi zawabu kubwa wakati atakaporudi.

KWELI BWANA WETU YESU KRISTO
NI MWOKOZI WA AJABU!